



KIBABII UNIVERSITY COLLEGE

UNIVERSITY EXAMINATIONS

**2014/2015 ACADEMIC YEAR
FOURTH YEAR FIRST SEMESTER**

SPECIAL / SUPPLEMENTARY EXAMINATION

FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

COURSE CODE: KIS 411

COURSE TITLE: KISWAHILI POETRY

DATE: THURSDAY 13TH AUGUST 2015

TIME: 11:30AM-1:30PM

MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee.

Swali la Kwanza ni la **lazima**

MUDA: Masaa Mawili (2)

KIBUCO observes ZERO tolerance to examinations cheating

1. (a) Fafanua sababu mbili wanazotoa wasawazishaji katika juhudhi za kuwapananisha wanajadi na wanamapinduzi. (alama 4)
- (b) Eleza ukitoa mifano sifa zozote tatu za ushairi katika kipindi cha urasimi mkongwe. (alama 6)
- (c) Soma shairi la “Sema” (Abdalla, 1970) kisha uleze bahari, muundo, matumizi ya lugha na maudhui yake. (alama 10)

Sema

Sema semea wajibu, ewe mwenye kutetema
Sema na walo karibu, na wa mbali ukisema
Sema kufunza wajibu, werevu au hekima
Sema asikie nani, mlimwengu asokoma

Sema yanayokukaa, yaliyo kukusakama
Sema yaliyozagaa, uwambie kuungama
Sema unajihadaa, wadhani yatawafuma?
Sema asikie nani, usiyejua kusema

Sema semea uasi, na hizi nyingi zahama
Sema toa wasiwasi, utarajie salama
Sema neno la risasi, lipenyalo likiuma
Sema asikie nani, usiyejua kusema

Sema yalo maakuli, maneno uloyapima
Sema tangaza halali, na haki ya kuandama
Sema toa mishikeli, usinong’one nguruma
Sema liwalo ni nini, ila kuzidi hasama?

Sema bila ya ukali, bembeleza ukisema
Sema neon la asali, wataramba wakitema
Sema tumia akili, kwao hukosi shutuma
Sema iwe jambo gani, mlimwengu asokoma

Sema na watoto wako, wawazaa uko wima
Sema au akhi yako, mlozaliwa na mama
Sema na sahibu wako, mlioshibana vyema
Sema lako hangaiko, waitafura hasama

Sema zitaje ghururi, dunia ni kama dema
Sema haiweki siri, inavuja ikitema
Sema dunia hatari, mtendayo yatuuma
Sema ajaliye nani, mlimwengu hana wema

Sema ‘Kwani hamuoni, wale waloachwa nyuma?
Sema wachuma tumboni, bila tija kusimama
Sema hayaonekani, yale uliyoyasema
Sema watia chumvini, matamu uliyochuma.

Sema na katu sisemi, kwa asojua kupima
Sema awe ni mtemi, asojua nilosema
Sema miko yangu mimi, sisemi neno daima
Sema niseme na nani, ili iweko salama?

- (d) Eleza maana ya idhini ya mshairi kisha ubainishe vipengele vyake vitatu muhimu kwa kutoa mifano ifaayo. (alama 6)
- (e) Eleza kwa kuzingatia hoja nne umuhimu wa ushairi. (alama 4)
2. Jadili ukitoa mifano mwafaka sababu zozote tano walizotumia wanausasa kupinga juhudzi za wanajadi za kudumisha mtindo wa mashairi ya kimapokeo. (alama 20)
3. Fafanua vigezo vitano vinavyotumiwa kuanisha bahari za mashairi ya Kiswahili. (alama 20)
4. Eleza sababu zozote tano zilizopelekea kuzuka kwa mgogoro katika ushairi wa Kiswahili mwaka 1970. (alama 20)
5. Jadili sababu tano za Euphrase Kezilahabi kutambulika kama mshairi maarufu. (alama 20)